Malaika –
Roho Zinazomhudumia Mungu

na

Ellis P. Forsman

Malaika –
Roho Zinazomhudumia Mungu

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 6, 2011

Malaika – Roho Zinazomhudumia Mungu

Luka 2:1-20

Nafikiri hakika itakuwa ni jambo la kutisha kama utashuhudia kutembelewa na malaika kwa mchungaji katika malisho. Lakini, je ukweli kwamba hatuwaoni malaika katika njia ambayo hawajionyeshi leo inamaanisha kwamba hawapo? Hapana, sijawahi kwenda London, lakini kunaukweli ambao haupingiki kwamba mji huu upo. Uchunguzi binafsi siyo mhimu kuamini katika, au kuelewa, malaika. Biblia inatufunulia vitu vingi kuhusu malaika kwa ajili ya uelewa wetu.

Wakati mwingine, hataivyo, mawazo potofu zinaaribu uelewa mzuri. Wabunifu wanaweka uelewa wao binafsi kuhusu malaika, ambayo watazamaji wengi isivyo sahihi wanakubali kuwa ni kweli.

Picha unazoona za malaika kimsingi ni mvuto wa wabunifu. Watu hawa wamedhamiria kuvutia na kuburudisha watoto pia imechangia watu kutokuelewa malaika. Hawa wanashughulika na ulimwengu wa kufikiria na ndoto.

Tunapaswa kutoa katika mawazo yetu sura za malaika kama tazamwa kupitia picha ambazo si sahihi na michoro ya kitoto. Badala yake tunapaswa kugeukia kurasa zilizo vuviwa za neno la Mungu, na hivyo tutakuwa tayari kupata picha halisi ya malaika, na jinsi wanavyotenda kazi.

Walipotokea

Malaika walitokea wapi? Wao siyo Mungu, vile vile pia siyo wanadamu.

Wao ni wa ukweli, viumbe hai wanaoshikilia nafasi ya kipekee. Ebr. 2:7, "*Umemfanya mdogo punde kuliko malaika, umemvika taji ya utukufu na heshima, umemtawaza juu ya kazi za mikono yako;*"

Yesu aliacha uwepo wa Mungu na kuchukua mfuno wa kibinadamu.

Kwa vile katika kuchukua mfano wa kibinadamu, katika kuchukua mfano huo alifanywa mdogo kuliko malika, tunaelewa kwamba malaika wanachukua sehemu kati ya Mungu na wanadamu. Wao siyo Mungu, pia siyo wanadamu, bali wapo katikati.

Watu wengi wanatazama malaika kama wanadamu wanaotukuzwa; hiyo ni, kama mtu mwenye haki anapokufa anafanyika malaika. Bila kujali inapendeza kiasi gain wazo hili linaweza kuonekana kwa

mwanadamu, haina msingi katika maandiko. Biblia inatuambia kwamba malaika ni viumbe vilivyoumbwa, na hawapo katika sehemu iliyoinuka ambapo mwanadamu mwenye haki anaweza kufikia. Neh. 9:6, "*Ezra akasema, wewe ndiwe BWANA wewe peke yako, wewe ulifanya mbingu, mbingu za mbingu, pamoja na jeshi lake lote,…*"

Tunaona katika msitari huu kwamba jeshi la mbinguni liliumbwa na Mungu.

Pia zingatia Kol. 1:15-17, "*Naye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote. Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni vitu vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka, vitu vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake. Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikamana katika yeye.*"

Tunahitimisha kutoka katika mistari hii kwamba malaika ni viumbe vilivyoumbwa: Zaburi 148:2, "*Msifuni enyi malaika wake wote; msifuni majeshi yake yote.*" Zaburi 148:5, "*Na vilisifu jina la BWANA, kwa maana aliamuru, vikaumbwa.*"

Kutokana na maandiko haya ni wazi kwamba malaika, kama mwanadamu katika mtazamo huu, ni viumbe vilivyoumbwa.

Asili yao

Malaika wanapaswa kuabudu, na siyo kuabudiwa.

Malaika wako chini kuliko Mungu na Kristo.

- 1 Pet. 3:22, "*Naye yupo mkono wa kuume wa Mungu, amekwenda zake mbinguni, malaika na enzi na nguvu zikiisha kutiishwa chini yake.*"
- Ebr. 1:6, "*Hata tena amletapo mzaliwa wa kwanza ulimwenguni, asema, na wamsujudu malaika wote wa Mungu.*"

Kwa vile malaika wako juu kuliko mwanadamu, je wanapaswa kuabudiwa na mwanadamu? Kol. 2:18, "*Mtu asiwanyang'anye thawabu yenu, kwa kunyenyekea kwa mapenzi yake mwenyewe tu, na kuabudu malaika, akijitia katika maono yake na kujivuna bure, kwa akili zake za kimwili.*"

Yohana alijifunza. Ufu. 22:8-9, "*Nami Yohana ndimi niliyeyasikia na kuyaona mambo hayo. Na hapo nilipoyasikia na kuyaona nilianguka, ili nisujudu mbele ya miguu ya malaika yule mwenye kunionyesha hayo. Naye akaniambia, angalia usifanye hivi; mimi ni mjoli wako, na wa ndugu*

zako manabii, na wale wayashikao maneno ya kitabu hiki. Msujudie Mungu."

Yohana alikuwa na makosa alipojaribu kuabudu malaika.

Tunaona, hivyo basi, kwamba malaika ni udhalili kwa Mungu, kwamba hawapaswi kuabudiwa, bali kwamba wanapaswa kumuabudu Mungu, sawa na sisi wanadamu.

Malaika ni mmoja mmoja katika asili.

Tabia nyingine ya kuelezea uasili wa malaika ni kwamba ni mmoja mmoja katika utambulisho. Malaika siyo tu mmoja wa wakuu, idadi inayotofautiana, bali ni binafsi, sawa na sisi wanadamu tulivyo mmoja mmoja.

Luka 1:19, "*Malaika akamjibu akamwambia, mimi ni Gabrieli, nisimamaye mbele za Mungu; nami nimetumwa niseme nawe, na kukupasha habari hizi njema.*"

Hapa malaika anaitwa kwa jina la Zakaria, ambaye angekuwa baba yake na Yohana mbatizaji.

Zingatia yafuatayo:

- Yuda 1:9, "*Lakini Mikaeli malaika mkuu, asiposhindana na ibilisi, na kuhojiana naye kwa ajili ya mwili wa Musa, hakuthubutu kumshitaki kwa kumlaumu, bali alisema Bwana na akukemee.*"

- Waamuzi 13:15-21, "*Kisha Manoa akamwambia huyo malaika wa BWANA, nakuomba tukuzuie, ili tupate kuandaa mwana mbuzi kwa ajili yako. Lakini malaika wa BWANA akamwambia Manoa, ujapokuwa wanizuia sitakula katika mkate wako; na kwamba watakakufanya tayari sadaka ya kuteketezwa, inakupasa kumsongezea BWANA. Kwa kuwa Manoa hakujua ya kwamba yeye ni malaika wa BWANA. Manoa akamwambia huyo malaika wa BWANA, jina lako ni nani, ili kwamba hap ohayo maneno yako yatakapotimia nipate kukutukuza? Huyo malaika wa BWANA akamwambia kwani wewe kuniuliza jina langu, kwa kuwa jina hilo ni la ajabu? Basi Manoa akamtwaa yule mwana mbuzi, pamoja na sadaka ya unga, akamtolea BWANA hapo juu ya mwamba; huyo malaika akatenda la ajabu; Manoa na mkewe wakaangalia. Kwa maana ikawa mara huo mwali wa moto ulipopaa juu mbinguni kutoka pale madhabahuni, huyo malaika wa BWANA akapaa katika mwali wa moto wa madhabahu; nao Manoa na mkewe wakaangalia; wakainama kifudifudi. Lakini malaika wa BWANA hakumtokea Manoa tena, wala mkewe. Ndipo Manoa alipojua ya kwamba ndiye malaika wa BWANA.*"

Malaika huyu alikuwa na jina, lakini alisema ilikuwa ni siri.

- "*Kwa nini unauliza jina langu, huoni ni la siri.*" (TMY).
- "Kwa nini unaniuliza jina? Ni zaidi ya uelewa" (NIV).

Neno la Kiebrania imetafsiri kama "siri" pia inamaanisha "vigumu sana."

Baadhi ya malaika wanachukua nafasi za juu kuliko wengine.

Kwa nyongeza katika majina ikionyesha tabia za kila mmoja, zaidi Biblia inatuambia kwamba malaika fulani wanatofautishwa kulingana na kuachana kwao.

Katika Yuda 1:9 hapo juu, Mikaeli aliitwa malaika mkuu.

Malaika hawana idadi.

Mat. 26:53, "*Ama wadhani ya kuwa mimi siwezi kumsihi Baba yangu naye atanileta sasa hivi zaidi ya majeshi kumi na wawili na malaika?*"

Kikosi kilikuwa kati ya elfu sita. Kama Mungu angetuma vikosi kumi na wawili wa malaika kwa ajili ya msaada wa Yesu, basi idadi ingekuwa malaika 72,000.

- Luka 2:13, "*Mara walikuwapo pamoja na huyo malaika, wingi wa jeshi la mbinguni, wakimsifu Mungu na kusema…*"
- Ufu. 5:11, "*Nikaona nikasikia sauti ya malaika wengi pande zote za kile kiti cha enzi, na za wale wenye uhai, na za wale wazee, na hesabu yai ilikuwa elfu kumi mara elfu kumi na elfu mara elfu.*"

10,000 mara 10,000 =100,000,000

1000 mara 1000 = 1,000,000 kwa kila 1000 mara 1000.

Hivyo idadi ya malaika waliozunguka kiti cha Mungu cha enzi ili zidi 1000,000,000 jumlisha 1,000,000

Ebr. 12:22, "*Bali ninyi mmeufikilia mlima Sayuni, mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu wa mbinguni, na majeshi ya malaika elfu nyingi,*"

Malaika ni roho.

Malaika siyo nyama mifupa au mwili unaohitaji mambo yake, kama jinsi tulivyo sisi wanadamu, bali ni roho. Kwa vile ni roho, hawana ukomo wa kuruka au kuwepo au kuhitaji mambo ya kimwili.

Malaika mara nyingine wanaweza kutokea bila kuonekana. Hesabu 22:27-31, "*Yule punda akamwona malaika wa BWANA, akajilaza chini ya*

Balaamu; hasira yake Balaamu ikawaka; akampiga punda kwa fimbo yake. BWANA akakifunua kinywa chake yule punda, naye akamwambia Balaamu nimekutenda nini hata ukanipiga mara tatu hizi? Balaamu akamwambia punda; kwa sababu umenidhihaki; laiti ningekuwa na upanga mkononi mwangu ningekuua sasa hivi. Yule punda akamwambia Balaamu, je! Mimi si punda wako, nawe umenipanda maisha yako yote hata leo? Nimezoea kukutenda hayo? Akasema la! Ndipo BWANA akafunua macho ya Balaamu akamwona malaika wa BWANA amesimama njiani, ana upanga mkononi mwake, umekwisha kufutwa naye akainama kichwa, akaanguka kifudifudi."

Kulikuwa na malaika ambaye mara ya kwanza alitokea bila kuonekana, lakini baadaye alionekana na Balaamu. Mwanzo 19:1, "*Basi wale malaika wawili wakaja Sodoma jioni; na Lutu alikuwa amekaa mlangoni pa Sodoma. Lutu akawaona akaondoka akaenda kuwalaki, akainama kifudifudi.*"

Majirani zake Lutu wali walielewa malaika kuwa ni binadamu. Mwanzo 19:5, "*Wakamwita Lutu, wakamwambia, wa wapi wale watu waliokuja kwako usiku huu? Uwatoe kwetu tupate kuwajua.*"

Malaika waliokuwa katika kaburi la Yesu wanaongelewa katika Marko 16:5 kama "*Kijana.*" Waamuzi 13:16, "*Lakini malaika wa BWANA akamwambia Manoa, ujapokuwa wanizuia sitakula katika mkate wako; na kwamba wataka kufanya tayari sadaka ya kuteketezwa, inakupasa kusongezea BWANA. Kwa kuwa Manoa hakujua ya kuwa yeye ni malaika wa BWANA.*"

Katika kupaa kwakw Yesu katika Matendo 1:10-11, malaika alitokea kama "*Wanaume … waliovaa kanzu.*"

Hivyo, malaika wanaweza kuonekana, pia wanaweza wasionekane, au wanaweza kuchukua mtazamo wa kibinadamu.

Malaika hawaoi wala kuzaa.

Marko 12:18-25, "*Kisha Masadukayo, watu wasemao ya kwamba hakuna kiyama, wakamwendea wakamwuliza na kusema, Mwalimu, Musa alituandikia ya kwamba ndugu ya mtu akifa, akamwacha mkewe hana mtoto, ndugu yake amtwae yule mkewe akampatie ndugu yake mzao. Bali kulikuwa na ndugu saba, wa kwanza akatwaa mke, akafa, asiache mzao. Wa pili naye akamtwaa akafa, wala yeye hakuacha mzao. Na wa tatu kadhalika; hata na wote saba, wasiache mzao, mwisho wa yote yule mwanamke akafa naye. . basi katika kiyama atakuwa mke wa yupi katika hao? Maana wote saba walikuwa naye. Yesu akajibu akawaambia, Je! Hampotei kwa kuwa hamyajui maandiko wala uweza wa Mungu? Kwa maana watakapofufuka katika wafu, hawaoi wala hawaolewi, bali huwa kama malaika walioko mbinguni.*"

Katika Mistari hii Yesu anafafanua kwamba malaika hawana uhusiano wa kijinsia, kama walivyo wanadamu.

Malaika hawausishwi na kifo.

Tabia nyingine ambayo si ya kawaida kwa mwanadamu ni kwamba malaika hawausishwi na kifo. Luka 20:34-36, "*Yesu akawaambia wana wa ulimwengu huu huoa na kuolewa; lakini wale wahesabiwao kuwa wamestahili kuupata ulimwengu ule, na kule kufufuka katika wafu hawaoi wala hawaolewi; wala hawawezi kufa tena; kwa sababu huwa sawasawa na malaika, nao ni wana wa Mungu, kwa vile walivyo wana wa ufufuo.*"

Malaika wanaweza kutenda dhambi na kupotea.

Petro ameeleza katika 2 Pet. 2:4, kwamba "*Kwa maana ikiwa Mungu hakuwaachilia malaika waliokosa, bali aliwatupa shimoni akawatia katika vifungo vya giza, walindwe hata ije hukumu.*"

Malaika wametenda dhambi na wakatupwa chini. Yuda 1:6, "*Na malaika wasioilinda enzi yao wenyewe, lakini wakayaacha makao yao yaliyowahusu, amewaweka katika vifungo vya milele chini ya giza kwa hukumu ya siku ile kuu.*"

Vifungu kama hivi vinatuonyesha wazi kwamba baadhi ya malaika walitenda dhambi, waliasi dhidi ya Mungu, walifuata mapenzi yao wenyewe, na walikataliwa na Mungu. Kama hali hii inaweza kuwapo miongoni mwa malaika, sasa kwa nini wengine wafikirie kwamba Wakristo hawawezi kutenda dhambi na kupotea?

Ufu. 12:7-9, "*Kulikuwa na vita mbinguni Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka naye akapigana pamoja na malaika zake; nao hawakushinda wala mahali pao hapakuonekana mbinguni. Yule joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye ibilisi na shetani, audanganyaye ulimwengu wote; akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye.*"

Kumbuka kwamba kifungu hiki kinaeleza kwamba ibilisi ana malaika zake mwenyewe. Malaika wanahusishwa na kuanguka kutoka katika sehemu yenye fadhila mbele za Mungu, na kutupwa kwao kutoka katika uwepo wake, na kupotea.

Misheni na kazi ya malaika wanaomtumikia Mungu.

Ebr. 1:13-14, "*Je yuko malaika aliyemwambia wakati wo wote, uketi mkono wangu wa kuume, hata nitakapoweka adui zako chini ya nyayo zako? Je hao wote si roho watumikao, wakitumwa kuwahudumu wale watakaourithi wokovu?*"

Malaika watumika kama wanaotumwa.

Njia moja wapo ambayo malaika utumika kwa ajili ya Mungu na kutumikia wanadamu ni pale wanapotumika kama wanaotumwa.

- Katika Luka 1:11-20, malaika alitoa ujumbe kwa Zakaria kwamba atakuwa na mtoto ambaye angetumika kama mtengeneza njia wa Yesu, Kristo. Kijana huyu alikuwa Yohana mbatizaji.
- Katika Luka 1:26-37, Malaika GAbrieli alimpa Mariamu taarifa kwamba atamzaa mtoto wa kiume ambaye ataitwa Yesu, na ambaye atatawala katika ufalme ambao hautakuwa na mwisho.
- Katika Luka 2:8-13, wachungaji pia walipewa taarifa na malaika kuhusu kuzaliwa kwa Kristo
- Malaika pia walitumika kama wanaotumwa katika kutangaza ufufuo katika Mat. 28:1-7.
- Kulikuwa na nyakati ambapo malaika alimtokea Paulo ili kumpa ujumbe. Matendo 27:22-24, "*Sasa nawapeni shauri, iweni na moyo mkuu, kwa maana hapana hata nafsi mmoja miongoni mwenu atakayepotea ila merikebu tu. Kwa maaa usiku huu wa leo malaika wa Mungu yule ambaye mimi ni wake, naye ndiye nimuabuduye, alisimama karibu nami, akaniambia usiogope Paulo hunabudi kusimama mbele ya Kaisari; tena tazama Mungu amekupa watu wote wanaosafiri pamoja nawe.*"

Malaika wanahudumu na tabia za mwili.

Unakumbuka tukio katika maisha ya Danieli iliyojumuisha kutupwa kwake katika tundu la samba. Katika Dan. 6:22, "*Mungu wangu amemtuma malaika wake, naye ameyafumba makanwa ya samba, nao hawakunidhuru; kwa kuwa mbele zake mimi nalionekana kuwa sina hatia; tena mbele yako Ee mfalme sikukosa neno.*"

Katika Matendo 12:7-10, malaika alitumika katika kumtoa Petro kifungoni.

Katika Luka 16:22, malaika wanaelezewa kuwa walimbeba Lazaro mwenye haki baada ya kifo chake hadi paradise.

Vifungu kama hivi vinaonyesha maana ya Zaburi 34:7, "*Malaika wa BWANA hufanya kituo, akiwazungukia wamchao na kuwaokoa.*"

Hapa inatokea katika vifungu vingi kuwa karibu binafsi kati ya malaika na wanadamu ambao wanalindwa.

- Mat. 18:10, "*Angalieni msidharau mmojawapo wadogo hawa; kwa maana nawaambia ya kwamba malaika wao mbinguni siku zote huutazama uso wa Baba yangu aliye mbinguni.*"
- 1 Kor. 11:7-10, "*Kwa maana kweli haimpasi mwanaume kufunika kichwa, kwa sababu yeye ni mfano wa utukufu wa Mungu. Lakini mwanamke ni utukufu wa mwanaume. Maana mwanamume hakutoka katika mwanamke, bali mwanamke katika mwanamume. Wala mwanamume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamke, bali mwanamke kwa ajili ya mwanamume. Kwa hiyo imempasa mwanamke awe na dalili ya kumilikiwa kichwani, kwa ajili ya malaika.*"

Neno "*kwa sababu ya malaika*" inamaanisha nini? Kitabu fulani kilieleza: "Kuelewa kifungu katika swali, itakuwa vizuri kama tukielewa nyingine mbili: Luka 15:7 na Efe 4:30. Yesu alieleza katika Luka, "*Kutakuwa na furaha mbinguni kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye…*" na Paulo katika Waefeso anasema, "*Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu.*" Kama kuna furaha mbinguni wakati mwenye dhambi anapotubu, na kama huzuni kwa Roho wa Mungu usababisha kutokutii, hivyo lazima malaika wanaotuhudumia wawe na furaha tunapomtii Mungu na kuhuzunika pale ambapo hatutii. Wakati wanawake Wakristo wanapoweka nywele zao isivyostahili, na hivyo kutojali mapenzi ya Mungu, hakika inaleta huzuni kwa malaika wanaowahudumia. Kwa sababu ya hii na shukrani kwa Mungu kwa ajili ya wema wake wa kuwatoa malaika ili watulinde, Wakristo kwa umakini lazima wadumishe mafundisho ya maandiko kwa kuzingatia nywele zao."

Kulingana na neno la Mungu, malaika wanaweza kututokea kwa mfano wa wanadamu, na hatuwezi kulitambua. Ebr. 13:2, "*Msisahau kuwafadhili wageni; maana kwa njia hii wengine wamewakaribisha malaika pasipokujua.*"

Hitimisho

Kwa vile malaika hawaonekani mara kwa mara kwa macho yetu ya kimwili, tunaweza kutojaribu kuangalia uwepo wao na umaana wao. Labda, baada ya somo hili tutakuwa na ujuzi mkubwa kuhusu malaika, roho hizo zinazohudumu wanaotumikia mapenzi ya Mungu katika maisha yetu.